
USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

# MIFUMO YETU

## Jarida la Mifumo ya TEHAMA ya TAMISEMI

TOLEO NA. 7 NOVEMBA 2018 — JANUARI 2019



# GoT-HOMIS

## Mfumo Madhubuti wa Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

*Wafamasia wa Hospitali ya Mkoa wa Mara, Deogratius John na Ester Muna wakitoa dawa kutoka Duka la Dawa la Hospitali kwa kutumia Mfumo wa GoT-HOMIS (Picha: Stephano Amoni, Mara)*

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*" Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), chini ya Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya*

*Ofisi ya Rais-TAMISEMI, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani"*

USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA**

# Bodi ya Uhariri

## Mwenyekiti

*Eng. Mussa Iyombe*
*Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## Wajumbe

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*

## Waandishi

*Atley Kuni – TAMISEMI*
*Melchiory Baltazary - TAMISEMI*
*Stephano Amon – Mara Mkoa*
*Athumani Pemba –Tanga CC*
*Jamadi Omari – Mtwara-Mikindani MC*
*Jacqueline Sombe – PS3*
*Gladys Mkuchu – PS3*

## Mhariri Mkuu

*Leah Mwainyekule – PS3*

## Wahariri

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*
*Jacqueline Sombe – PS3*
*Gladys Mkuchu – PS3*
*Conrad Mbuya – PS3*

## Msanifu Kurasa

*Gladys Mkuchu – PS3*



## Jarida hili hutolewa na:

*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI*
*S.L.P 1923*
*Dodoma-Tanzania*
*Simu: (+255) 26 -2321234*
*Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz*
*Tovuti: www.tamisemi.go.tz*
*Blogu: blog.tamisemi.go.tz*
*Facebook: Ofisi ya Rais – TAMISEMI*
*Instagram: ortamisemi*

## Ndani ya Jarida Hili:

**Tahariri……………………………………………………………………………………….......uk 6**

**Hatua Muhimu za Mfumo wa GoT-HOMIS…………………………………………………...uk 7**

**LAN Kuwezesha Utendaji Kazi wa Mfumo wa GoT-HOMIS ……….…………………….…..uk 8**

**GoT-HOMIS Kuziba Mianya ya Ubadhirifu ………. ..……………...……...………..…....uk 9**

**PS3, TAMISEMI Wakili wa Mfumo wa Usimamizi Vituo vya Afya………………………...uk 10**

**TEHAMA Yachochea Uboreshwaji wa Huduma za Afya…………...………………………..uk 11**

**Matumizi ya GoT-HoMIS Yaleta Tija Mara……………...………..……………………...………...uk 12**

**GoT-HOMIS Chanzo cha Ongezeko la Mapato Kituo cha Afya….………..…………...…….uk 13**

**Teknolojia Yaleta Mabadiliko Chanya Sekta ya Afya Tanga……………...……..…...…...….uk 14**

## *TAHARIRI:*

# Matumizi ya GoT-HoMIS Msingi wa Huduma Bora za Afya

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) ina jukumu la kuimarisha usimamizi wa utoaji wa huduma bora kwa wananchi kupitia mifumo ya TEHAMA. Moja kati ya mifumo hiyo ni mfumo wa *Government of Tanzania – Health Operationts Management Information System (*GoT-HOMIS) ambao ni wa kielektroniki na umewekwa kwa lengo la usimamizi wa shughuli za uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya hapa nchini.

Kufungwa kwa mfumo huu na kuanza kutumika itasaidia kurahisisha shughuli za vituo vya kutolea huduma za afya na kusimamia uzalishaji na uhifadhi sahihi wa taarifa na takwimu za wagonjwa na magonjwa, mapato na dawa za vituo vya kutolea huduma za afya.

Mfumo wa GoT-HOMIS utasaidia vilevile katika kuboresha huduma za afya nchini na kuleta tija ya upatikanaji wa haraka wa takwimu mbalimbali na kwa wakati, na kusaidia kujua matumizi ya dawa hadi ngazi ya mtoa huduma.

Aidha, mfumo wa GoT-HOMIS utachochea ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya kituo, kwani mfumo huu utaonesha mapato sahihi ambayo yanakusanywa na kituo husika. Faida nyingine ya mfumo huu ni kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, kupunguza gharama za upatikanaji wa taarifa, kuongeza uwajibikaji, upatikanaji wa taarifa sahihi kwaajili ya kufanya maamuzi kwa wakati.

Pamoja na faida zinazopatikana kupitia mfumo wa GoTHOMIS mfumo umeweza kuunganishwa na mfumo wa Bima ya Afya (NHIF) ili taarifa za mteja/mwanachama ziweze kuhakikiwa na kukiwezesha kituo cha kutolea huduma kulipwa madai yake na NHIF bila usumbufu.

Naomba nitoe rai kwa vituo vya kutolea huduma za afya ambavyo bado havijafunga mfumo huu kuhakikisha kwamba vinanunua vifaa vitakavyowezesha mfumo kufungwa na kufanya kazi yake kama ilivyokusudiwa.

Ofisi ya Rais TAMISEMI inatarajia kwamba vituo vyote 367 vya kutolea huduma za afya vitafunga na kutumia mfumo huu kama ilivyoelekezwa na kama inavyotarajiwa, ili kuwezesha ufanisi katika upatikanaji wa taarifa na utoaji wa huduma za afya nchini.

Naomba niwatakie usomaji mwema wa jarida hili, na kwa pamoja tuendeleze gurudumu la maendeleo katika uboreshaji wa mifumo.


Asanteni sana.



**Eng. Mussa I. Iyombe**

**Katibu Mkuu**

# Hatua Muhimu za Mfumo wa GoT-HOMIS




Mfumo wa *Government of Tanzania – Health Operations Management Information System* (GoT-HOMIS) umepitia hatua mbalimbali za matoleo na maboresho hadi kufikia toleo la tatu lililoanza kutumika kuanzia mwishoni mwa mwaka 2017.

Matoleo na maboresho hayo yalijikita katika kuongeza wigo wa matumizi ya mfumo katika vituo vya kutolea huduma za Afya, kuboresha ufanisi wa mfumo, kuboresha taarifa zinazokusanywa, kuongeza usalama wa taarifa na kuunganishwa na mifumo mingine ya kisekta na kimkakati.

Katika juhudi za kuongeza ari ya umiliki na utumiaji wa mfumo, wadau mbalimbali kutoka katika ngazi tofauti tofauti hadi katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma wamekuwa wakishirikishwa katika maboresho ya mfumo huu.

Juhudi hizi pia zimesaidiwa na mafunzo katika eneo la kufanyia kazi (*onsite training*), kupokea na kufanyia kazi mapendekezo ya watumiaji na wataalamu kusikiliza na kutatu changamoto zinazotolewa taarifa na watumiaji wa mfumo katika vituo vya kutolea huduma.

Katika mwaka 2018, Mfumo wa GoT-HOMIS uliboreshwa na kupata ingizo la program maalumu za Kifua Kikuu (TB), Huduma ya Mama na Mtoto (RCH), na Huduma za VVU (CTC).

Kazi hii iliyofanywa na OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imechangia kuondoa uwepo wa mifumo mingi katika vituo vya kutolea huduma za Afya na badala yake kituo kufunzwa, kufunga na kutumia mfumo mmoja tu wenye mahitaji yote ya taarifa na shuhuli za uendeshaji wa kituo.

Pia, mfumo wa GoT-HOMIS umeunganishwa na Muungano Gateway ambayo ni kama bomba la mawasiliano kwa mifumo yote iliyo chini ya OR-TAMISEMI kuiwezesha kuwasiliana na mifumo mingine iliyo nje ya Wizara.

Pamoja na maboresho yote yaliyokwisha fanyika katika mfumo wa GoT-HOMIS wataalamu wa mfumo huu wamekuwa wakiendelea kufanyia kazi mapendekezo mapya ya watumiaji, mabadiliko ya teknolojia na miongozo ama kanuni mpya katika utunzaji na usafirishaji wa data za kitabibu kwa njia za kielektroniki.

***Melchiory Baltazary - TAMISEMI***

# LAN Kuwezesha Utendaji Kazi wa Mfumo wa GoT-HOMIS

Mwanza ni moja kati ya mikoa 26 nchini ambayo moja ya Halmashauri zake (Ilemela MC) imenufaika kwa kufungiwa mfumo wa GoT-HOMIS katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya.

Mkoa huu pia unanufaika na fedha za malipo kwa ufanisi, ijulikanayo kama Results Based Financing (RBF), na kupitia fedha hizo vituo vyote vya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela vimeweza kufungiwa mtandao kiambo ambao utawezesha ufanyaji kazi wa haraka wa mifumo, ikiwemo GoT-HOMIS.



*Afisa kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela akifunga mfumo wa GoT-HOMIS katika Zahanati ya Pasiansi mkoani Mwanza (Picha: Jacqueline Sombe, PS3)*

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, John Paul Wanga, anasema kwamba uwekaji wa mtandao kiambo katika vituo vya kutolea huduma za afya ni matokeo ya maagizo kutoka OR-TAMISEMI kupitia Waziri wake, Mhe. Selemani Jafo, ambaye aliagiza vituo vyote vya kutolea huduma za afya kufunga mfumo wa GoT-HOMIS. Kutokana na agizo hilo, Manispaa ya Ilemela ilijizatiti kulitekeleza.

"Tuna matarajio makubwa kwamba mfumo utatuwezesha kufanya uchambuzi hasa wa magonjwa ambukizi, na kama Serikali tutaweza kutambua ugonjwa umesambaa kwa kiasi gani na wagonjwa wangapi wamehudumiwa kwa muda wa robo mwaka na kwa mwaka," anaeleza Wanga, na kuongeza: "Itatuwezesha pia kutambua tumetumia fedha kiasi gani katika kuboresha huduma za afya, na tumeongeza mapato kwa kiasi gani."

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, Halmashauri yake haikuwa na sifa nzuri sana katika sekta ya afya, na ndio maana wameamua pia kutatua changamoto walizokuwa nazo hapo awali. "Tutafuatilia uadilifu wa maafisa katika kuusimamia mfumo, kusimamia mapato yanayokusanywa vituoni, kuboresha usimamizi pamoja na ongezeko la wateja. Maafisa watatakiwa kufanya kazi kwa kufuata mahitaji ya mfumo, na pia tutaandaa mkataba wa utendaji kazi kwa maafisa. Yote haya ni katika kuboresha huduma," anasisitiza Wanga.

Dkt. Florian Tinuga ambaye ni Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza, anaeleza kwamba hali ilikuwa mbaya sana kwa Halmashauri hiyo hapo awali.

"Wala hata si jambo zuri kufikiria. Tangu nimefika katika Halmashauri hii mwezi Oktoba 2017 nikitokea Kasulu, Kigoma, kati ya masuala ambayo yalikuwa yananiumiza kichwa ni utendaji kazi hafifu wa vituo vya kutolea huduma za vituo vya afya vya Serikali. Hili lilisababisha Ilemela kuwa kati ya Halmashauri 20 zisizofanya vizuri kwa upande wa sekta ya afya, na hili lilitajwa katika ripoti ya mwaka ya MTUHA, ambapo Ilemela ilikuwa ya 163 kati ya Halmashauri 184," anaeleza.

Kwa mujibu wa Dkt. Tinuga, hakuna mtu aliyetamani kuwa na uongozi au kuwa mjumbe wa kamati za afya katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. Hawakukata tamaa, bali waliamua kufanya kazi kwa pamoja na kuja na mikakati ya kuboresha huduma ambapo mkakati mkubwa ulionekana kuwa ni kuweka mtandao kiambo ambao utawezesha kuunganisha mifumo muhimu ya afya kama GoT-HOMIS na DHIS2.

***Inaendelea uk. 15***

# GoT-HOMIS Kuziba Mianya ya Ubadhirifu

Mfumo wa Kieletroniki kwa ajili ya Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Tanzania *Government of Tanzania – Health Operations Management Information System* (GoT-HOMIS) unaelezwa kuwa chachu ya kuleta suluhisho katika ngazi ya wafanya maamuzi na kutatua tatizo sugu la upatikanaji wa taarifa za vituo vya matibabu kwa usahihi na kwa wakati, endapo utatumika ipasavyo.

Joel Deogratius Mazigo ambaye ni Afisa TEHAMA wa OR-TAMISEMI, anasema kwamba mipango mingi ya Serikali ilikuwa ikikwama kutokana na fedha nyingi kuishia mikononi mwa watu wachache wasiokuwa waaminifu. Hilo linatokana na ukusanyaji hafifu wa mapato, ubadhirifu pamoja na udanganyifu.

Kabla ya kuanza kutumika kwa mfumo wa GoT-HOMIS hospitali zote za Serikali nchini zilikuwa zikitumia stakabadhi ambazo zilitolewa na Wizara ya Afya, ambapo katika stakabadhi hizo kiwango cha tozo kilikuwa kimechapishwa kwa mashine moja kwa moja. Hali hiyo ilichangia watu kufanya udanganyifu wa kutumia vitabu mbadala ambavyo walivichapisha kwa kificho na kisha kuviingiza kinyemela hospitalini.

Ilikuwa ni vigumu kuusambaza mfumo kwenye maeneo mengi ya utoaji huduma za afya bila kuwa na sera mahususi. Baada ya sera hiyo kutungwa, mfumo ulisamabazwa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati katika maeneo mengine nchini.

Kwa mujibu wa Mazigo, mara baada ya mfumo huo kuanza kutumika katika hospitali ya Tumbi na kuonesha mafanikio, ulisambazwa katika hospitali zingine za mikoa ikiwepo Sekou Toure Mwanza, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa pamoja na zingine. Hilo liliwezesha kutambua takwimu za hospitali, lakini pia liliinua mapato katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya ambavyo tayari vilikuwa vimeanza kutumia huu mfumo.

Mpaka Novemba 2018 mfumo huu umeshasimikwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo 355, zikiwemo Hospitali za Rufaa za Mikoa 23, Hospitali za Wilaya 76, Hospitali Teule za Wilaya 11, Vituo vya Afya 155 na Zahanati 90 kote nchini.



*Afisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi, Nkinda Shekalago, akizungumzia mfumo wa GoT-HOMIS Dodoma (Picha: Atley Kuni, TAMISEMI)*

Mtaalam huyo anaendelea kusema kwamba kutumika kwa mfumo wa GoT-HOMIS kumesaidia kutambua mahitaji ya kila eneo la nchi na mahitaji ya msingi, husasan katika mgawanyo wa rasilimali za vifaa tiba pamoja na dawa kulingana na jiografia ya nchi na magonjwa yaliyo sugu katika eneo husika.

Afisa Ustawi Mwandamizi kutoka OR-TAMISEMI, Nkinda Shekalago, anasema kwamba wakati akifanya kazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma kipindi cha nyuma, walilazimika kutafuta mzabuni wa kuunda mfumo ili kusaidia shughuli ya uendeshaji wa huduma za afya kwenye hospitali hiyo.

"Nakumbuka kabla ya kuanza kwa mfumo wa GoT-HOMIS sisi kama hospitali ya mkoa tulifanya jitihada binafsi za kutafuta kampuni ambayo ingeunda mfumo wa kusaidia shughuli za uendeshaji wa mambo ya afya ambapo tulimpata mtengenezaji wa mfumo aliyeunda mfumo uliojulikana kwa jina la GPITG. Hata hivyo suala la uendeshaji mfumo lilikuwa ni shida kutokana na mtengenezaji kutokuwa mwajiriwa, hivyo kuleta shida pindi tulipohitaji kufanya marekebisho," anasema Nkinda.

Anaongeza kwamba mfumo wa GoT-HOMIS ulipoanza, ilileta mabadiliko makubwa ikilinganishwa na mfumo uliobuniwa hapo awali.

"Sisi tuliokuwa wadau wa mwanzo kabisa tunaona tofauti kubwa sana baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa GoT-HOMIS hasa upatikanaji wa takwimu na taarifa ambazo zimesaidia katika maamuzi kwa kutambua mahitaji halisi ya kituo, ikiwepo dawa na vifaa-tiba vingine.


***Inaendelea uk. 10***

# GoT-HOMIS Kuziba Mianya

*Inatoka uk. 9*

Mapema mwezi Agosti 2018, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Selemani Jafo, akihojiwa katika kipindi maalum cha *Tunatekeleza* kinachorushwa na Televisheni ya Taifa (TBC), alikaririwa akisema kwamba ufungaji wa mifumo umesaidia katika ongezeko la mapato na kuziba mianya ya udanganyifu.

"Katika kipindi cha mwezi mmoja, kwenye hospitali zetu za wilaya tulikuwa tunakusanya Shilingi Milioni 3 hadi 6, lakini sasa baada ya kufunga mifumo maalum ikiwepo GoT-HOMIS makusanyo yameongezeka na kufikia kati ya Milioni 24 hadi 40 kwa mwezi. Lakini pia upatikanaji wa taarifa umekuwa rahisi, na hali hii sasa itasaidia katika kufanya mipango yetu ya uboreshaji wa huduma za afya kuwa madhubuti," alieleza.




Mfumo wa GoT-HOMIS unaonekana kuwa suluhisho la kadhia ya muda mrefu, ambapo kila Hospitali ya Mkoa nchini ilikuwa inatafuta namna ya kujikwamua na kupata njia sahihi ya kuendesha huduma za afya katika maeneo yao.

Ili kuhakikisha uendelevu wa mfumo huu, OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), chini ya ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), wameendelea na jitihada za kuimarisha mifumo na kuwajengea uwezo wataalam mbalimbali ili waweze kuuhudumia mfumo katika maeneo ya kutolea huduma za afya.

# PS3, TAMISEMI Wakili wa Mfumo wa Usimamizi Vituo vya Afya

"GoT-HOMIS ni mfumo ambao unatumika na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia mgonjwa anapofika kituoni na kusajiliwa mpaka anapomaliza kupata huduma. Mfumo wa GoT-HOMIS unahusisha idara zote katika hatua za kitibabu ndani ya vituo vya kutolea huduma za afya," anasema Revocatus Mtesigwa, Meneja wa Mifumo ya TEHAMA katika Mradi wa Uimarishwaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).

Mtesigwa anasema kwamba OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na PS3 wamewezesha uundwaji wa mfumo wa GoT-HOMIS ambao utakuwa rahisi kwa matumizi. Mfumo umeandaliwa kuwa na uwezo wa kufanya kazi hata pasipo na mtandao, na hivyo kuweza kutoa huduma wakati wowote na kwa haraka. Hii pia inasaidia kutoahirisha utoaji wa huduma kama ilivyo kwa mifumo mingine pale ambapo kunakuwa na tatizo la mtandao.

GoT-HOMIS itahitaji kutumia mtandao pale ambapo taarifa zitatakiwa kutumwa kwenda OR-TAMISEMI mara moja kila mwezi, na hivyo italazimu kituo kutumia mtandao wakati huo.

Kwa mujibu wa Mtesigwa, vituo vya afya vyenye changamoto za mtandao vitalazimika kuunganisha mtandao kwa ajili ya kutuma taarifa hizo mara moja tu kwa mwezi.

OR-TAMISEMI vilevile itakuwa na dashibodi ambayo itakuwa inahuisha taarifa zote za vituo vyote vilivyounganishwa na mfumo wa GoTHOMIS na hii itasaidia kuwa na taarifa za wagonjwa zilizojitosheleza. Halikadhalika, faida kubwa itokanayo na hili ni kwamba mgonjwa atakapokwenda kwenye vituo tofauti ambavyo vina mfumo huu, taarifa zake za mwisho zinaweza kuonekana kokote na kusaidia kutambua historia ya mgonjwa, jambo litakalorahisisha uendelezaji wa matibabu.

"Hii imetatua changamoto zilizokuwa awali ambapo taarifa za mgonjwa zilikuwa zinajirudia-rudia na hivyo kuwa ngumu kutoa takwimu sahihi za magonjwa na idadi ya wagonjwa," anafafanua Mtesigwa.

*Inaendelea uk. 16*

# TEHAMA Yachochea Uboreshwaji wa Huduma za Afya

Utumiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kutoa huduma kwa wananchi umekuwa ni kiu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda mrefu. Ni miaka michache tu iliyopita utumiaji wa TEHAMA katika vituo vya kutolea huduma za afya haukuonekana kuwa na umuhimu au ulazima sana, na vituo vichache vimekuwa vikitumia kompyuta huku vingine vikiwa havina kabisa kitendea kazi hicho.

Ili kuboresha huduma na kuwa na usimamizi madhubuti wa shughuli za vituo vya kutolea huduma za afya, Serikali kupitia OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) inaendelea kuhakikisha kila kituo cha kutolea huduma za afya nchini kina mfumo wa kieletroniki wa GoT-HOMIS ambao unasaidia kuweka taarifa sahihi za vituo, ikiwemo idadi ya wagonjwa waliopata aina ya huduma iliyotolewa na dawa zinazotolewa kwao.

Kwa upande wa vituo, mfumo huu utachangia kuongezeka kwa mapato na kupunguza matumizi ya karatasi ambayo hutumia muda mwingi na kupoteza rasilimali nyingi.

"Kwa zahanati kuwa na mfumo unaoshughulika na kusimamia shughuli zote zinazofanyika pamoja na kuhifadhi taarifa za kila hatua, si jambo la masihara," anaeleza Brigitha Machumbe, ambaye ni Mganga Mfawidhi katika Zahanati ya Pasiansi, Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza.

Kwa mujibu wa Machumbe, moja ya changamoto walizowahi kukutana nazo kwa kutokuwa na mfumo mzuri wa usimamizi ni ukusanyaji hafifu wa mapato. Anasema: "Kila kituo cha kutolea huduma za afya hutoa huduma bure kwa watoto chini ya miaka mitano, wajawazito, na wazee kuanzia miaka sitini. Katika hili suala la wazee, imetokea mara nyingi kwamba mtu anaweza kuja na kusema ana miaka 60 lakini kiuhalisia yuko chini ya umri huo, na hana hata kadi ya wazee. Kutokuwa na mfumo kunasababisha changamoto zaidi, kwani hukuna taarifa za kuthibitisha ukweli wa taarifa ya aliyejiita mzee, hivyo kusababisha utoaji wa huduma bila kuwa na uhakika wa taarifa."




*Muuguzi wa Zahanati ya Pasiansi iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza, Neema Meela, akieleza namna mfumo wa GoT-HOMIS utakavyorahisisha kazi na kuokoa muda. (Picha: Jacqueline Sombe, PS3)*

"Mimi ni shahidi na muathirika wa taarifa hafifu za Mfumo wa Takwimu wa Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA), ambapo taarifa zinasoma tofauti kati ya kilichoandikwa katika rejesta, na matokeo ya mwisho katika mfumo wa MTUHA, anaeleza Asumpta Mwijage, ambaye ni Afisa Muuguzi Msaidizi katika zahanati hiyo ya Pasiansi. "Nimefanya kazi hapa kwa takribani miaka mitatu, na kwa muda wote huo nimeona utendaji kazi ukiwa na changamoto kubwa," anasema.

Kwa sasa anaamini kwamba kwa kuwepo mfumo wa GoT-HOMIS fedha za malipo kwa ufanisi (RBF) zinazotolewa na Benki ya Dunia zitaongezeka, hasa kutokana na ukweli kwamba kutakuwa na taarifa zinazoeleweka zitakazotokana na rejesta iliyopo kwa kielekroniki.

"Nina watoto na familia ya kuiangalia, lakini muda wa ziada najikuta naupoteza kazini hivyo kukosa muda mzuri na familia yangu; na kwakuwa tulikuwa na mifumo duni ya kufanyia kazi, ilitupasa kuingiza taarifa za kila siku kwenye rejesta kila baada ya kazi muda wa jioni baada ya kumaliza kuhudumia wagonjwa, anasimulia Neema Meela, muuguzi katika Zahanati ya Pasiansi. Anaongeza: "Matarajio yangu naweza kusema kuwa hata kama nitakaa muda wa ziada kama zamani, kwa sasa kutakuwa na unafuu kwani hakutakuwa na changamoto ya ucheleweshwaji wa posho za muda wa ziada, kwasababu fedha za RBF zitaongezeka na kutupa motisha."

"Hali haikuwa ya kuridhisha hapa Zahanati ya Pasiansi, unakuja kupata huduma unasuburi zaidi ya saa moja huku unamuona muhudumu anatoka chumba kimoja kuingia kingine, natumaini hali hii itapungua au kuisha kabisa," anasema Ibrahim akiwa zahanati hapo kupata huduma.

Zahanati ya Pasiansi ni moja kati ya vituo vya huduma za afya nchini ambavyo vimenufaika na uwekaji wa mtandao kiambo LAN ambao unatarajiwa kuwa kichochezi cha kuboresha huduma kwa wananchi kupitia mfumo wa GoT-HOMIS pamoja ka kuboresha taarifa za Mfumo wa Takwimu wa Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA).

***Jacqueline Sombe, PS3***

# Matumizi ya GoT-HOMIS Yaleta Tija Mara

Matumizi ya Mfumo wa Afya wa Serikali ya Tanzania, ujulikanao kama GoTHOMIS yamekuwa na tija na faida kubwa sana katika Hospitali ya Mkoa wa Mara. Mfumo wa GoT-HoMIS umesaidia kutunza taarifa mbalimbali kama vile wagonjwa, dawa, vifaa tiba pamoja na kuongeza mapato.

"Hospitali imeongeza mapato yatokanayo na malipo ya wateja '*user fee*' kutoka sh milioni 28 hadi milioni 47 kwa mwezi, hali ambayo inaifanya hospitali kuweza kuwa na fedha za kutosha kuboresha utoaji wa huduma za afya," anasema Mhasibu wa Hospitali ya Mkoa wa Mara, Mpuya Agustino Sendo.

Sendo anaeleza kwamba matumizi ya mfumo wa GoT-HOMIS kwa sasa ndio njia mbadala ya kukabiliana na upotevu wa mapato, vifaa tiba pamoja na dawa. Hali hii inasaidia kuondoa usumbufu kwa wateja wanaofika kupata huduma hospitalini kwa kukosa dawa na vifaa tiba, kwakuwa hospitali itakuwa na fedha za kuweza kununua mahitaji hayo. Kabla ya kuwa na mfumo, udhibiti wa fedha, dawa na vifaa tiba ulikuwa mgumu sana na kusababisha mapato mengi kupotea mikononi mwa watu wasio waaminifu.

Naye Afisa Ustawi wa Jamii wa hospitali hiyo, Maulid Kitumbo, anasema kwamba kabla ya mfumo wa GoTHOMIS, utaratibu wa utoaji msamaha kwa wateja wasiokuwa na uwezo ulikuwa mgumu kutekelezeka kwakuwa wakati mwingine ilishindikana kubaini ukweli kutokana na wengine kutoa taarifa zisizo sahihi.

Kwa kutumia mfumo, mteja wa msamaha anatambulika kwa namba maalum na anapunguziwa usumbufu kupitia sehemu ambazo hatakiwi kupitia katika utaratibu wa kupata huduma, kwani taarifa zake zinakuwa zimefika sehemu zote muhimu kabla ya yeye kwenda huko.


"Si rahisi kufanya udanganyifu kwa kutoa huduma ya kulipia kwa mteja wa msamaha, maana mfumo hauwezi kuruhusu huduma hiyo itolewe bure. Kwa kutumia mfumo, ni rahisi kutenganisha huduma zinazotolewa kwa msamaha na zile ambazo lazima kulipia, anaeleza Kitumbo na kuongeza: "Hali hii imerahisisha kazi zangu na kuongeza: mapato kwa kiasi fulani kwenye hospitali yetu kwa kudhibiti misamaha isiyokidhi matakwa ya kisera."

Akizungumzia manufaa ya mfumo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa wa Mara, Dkt Joachim Eyembe, anapongeza jitihada za Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kwa kupitia mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), kwa kufanikisha ufungaji wa mfumo huu.

Mfumo unasaidia kubadili utendaji kazi wa watumishi kuwa rahisi zaidi, kuongeza uwazi, kuboresha utoaji huduma, na kupunguza malalamiko kutoka kwa wananchi. Kwa kuanzia, anaeleza Dkt. Eyembe, mfumo unatumika katika idara chache, lakini idara zote zilizobaki nazo zitaanza kutumia mfumo haraka iwezekanavyo punde kompyuta zitakaponunuliwa hivi karibuni.

"Matumizi ya Mfumo wa GoT-HOMIS ni maagizo ya Serikali kuwa Hospitali za Mikoa, Wilaya, Zahanati na Vituo vya Afya kuhakikisha wanatumia mfumo kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za afya. Hatuna budi kutekeleza maagizo ya Serikali, kwani ni moja ya mkakati wa kuboresha utoaji huduma kupitia matumizi ya mifumo ya kielektroniki," anahitimisha Dkt Eyembe.

***Stephano Amoni, Mara Mkoa***



***Mhasibu wa Hospitali ya Mkoa wa Mara, Christina Mwita, akiwahudumia wagonjwa wanaolipia huduma mbalimbali zinazopatikana hospitali kwa kutumia mfumo wa GoT-HOMIS (Picha: Stephano Amoni, Mara Mkoa).***

# GoT-HOMIS: Chanzo cha Ongezeko la Mapato Kituo cha Afya Likombe

Kituo cha Afya Likombe kilichopo Manispaa ya Mtwara-Mikindani, kimepiga hatua kubwa katika maboresho ya utoaji wa huduma za afya baada ya kuanza kutumia mfumo wa GoT-HOMIS.

Mfumo huu ulioanza kutumika mwezi Mei mwaka huu umefanya kituo hicho kuwa na ongezeko la mapato kutoka milioni 4, hadi milioni 6 kwa mwezi katika fedha za papo kwa papo. Aidha, fedha za wagonjwa wanaotibiwa kupitia mfuko wa Bima ya Afya zimeongezeka kutoka shilingi milioni 8 hadi shilingi milioni 16 kwa mwezi, na kufanya kituo hicho kukusanya zaidi ya shilingi milioni 20 kwa mwezi.

Hayo yamesemwa na Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dkt. Nuru Hatibu, alipotembelewa ofisini kwake, na kueleza kuwa kutokana na ongezeko la mapato, kituo kimeweza kujihakikishia upatikanaji wa dawa kwa asilimia mia moja.

"Tumefanikiwa kudhibiti mianya ya upotevu wa dawa. Kwa sasa kituo chetu hakina upungufu wa dawa na hakuna mgonjwa anayefika kituoni akakosa dawa," anahakikisha Dkt. Nuru.

Aidha, mapato hayo yamewezesha kituo kuwalipa wafanyakazi fedha ya masaa ya ziada na '*on call allowance*' kwa wakati, hali ambayo imesababisha wafanyakazi kufanya kazi kwa kujituma na kusababisha kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa kwenye kituo hicho.

"Kabla mfumo huu haujafungwa, kituo kilikuwa kinahudumia wagonjwa wapatao 70 hadi 80 kwa siku upande wa wagonjwa wa nje *'OPD'* lakini kwa sasa kituo kinahudumia wagonjwa 150 kwa siku. Halikadhalika, wagonjwa waliokuwa wakihudumiwa kwenye wodi ya wazazi walikuwa wastani wa wagonjwa 80 kwa mwezi, na kwa sasa idadi hiyo imeongezeka na kufikia wastani wa wagonjwa 200 kwa mwezi. Wagonjwa wengine hawa wanatokea vijiji vilivyoko Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, vikiwemo vjiji vya Msanga Mkuu, Ziwani, Msimbati, Tangazo na Utende ambao wamefurahishwa na huduma bora inayotolewa kwa sasa," anaongeza Dkt Nuru.




***Baadhi ya wagonjwa wakisubiri kupata huduma katika kituo cha Likombe (Picha: Jamadi Omari, Mtwara-Mikindani MC)***

Pamoja na faida hizo, mfumo huu pia umerahisisha utunzaji wa data na upatikanaji wa taarifa za wagonjwa na taarifa mbalimbali kwa wakati. Aidha kituo kimeweza kutenga bajeti ya shilingi milioni 3 kwa ajili ya ukarabati mdogo wa jengo la wagonjwa wa nje.

Someo Ismail mkazi wa Magomeni Mtwara anaishukuru Serikali kwa kuanzisha mfumo huo wa GoT-HOMIS kwani ana imani kwamba kwa sasa fedha zote zinaingia Serikalini na kuboresha huduma za afya. Aidha, amewashukuru wafanyakazi wa Likombe kwa huduma nzuri alizozipata.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Manispaa, Dkt. Joseph Kisala, ameishukuru Serikali kwa kuleta mfumo huo. Amewataka wananchi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani kuamini tiba za kitaalam katika vituo na zahanati zilizopo kwani wamejipanga kuhakikisha changamoto zote zinatatuliwa kwa wakati.

Manispaa ya Mtwara-Mikindani ina jumla ya vituo saba vya Serikali vinavyotoa huduma za afya, kati ya hivyo vituo vinne vimeshafungwa mfumo wa GoT-HoMIS na imedhamiria kukamilisha kufunga mfumo huo kwa vituo vitatu vilivyobaki ifikapo Januari 2019.

***Jamadi Omari, Mtwara-Mikindani MC***

# Teknolojia Yaleta Mabadiliko Chanya Sekta ya Afya Tanga

Mabadiliko ya teknolojia yamekuwa ni chachu kubwa katika kuboresha huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya. Kama ilivyo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nyingine nchini, vituo vya kutolea huduma za afya katika Halmashauri ya Jiji la Tanga vimeshudia mabadiliko makubwa ambayo yametokana na kuanzishwa kwa mfumo wa usimamizi katika vituo vya kutolea huduma za afya ,unaojulikana kama GoT-HOMIS.

"Kwanza kabisa, mfumo wa GoT-HOMIS unatuwezesha kupata taarifa sahihi na za wakati, taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo huwa zinakuwa salama na hazifutiki. Pindi mgonjwa anapoingiziwa taarifa zake kwenye mfumo, inakuwa rahisi kupata historia yake anapotembelea siku nyingine hata kama atakuwa amepoteza kadi au kusahau namba yake ya utambulisho. Kwa kuwa taarifa zinaingizwa kwenye mfumo kwa usahihi, kupata taarifa nyingine za kitakwimu kama MTUHA inakuwa rahisi na kwa haraka mno; *it's a single click process,"* anasema Dkt. Angelina Mashaka, Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Ngamiani.

Vilevile, anaeleza, matumizi ya mfumo wa GoT-HOMIS yanasaidia kufahamu idadi ya wagonjwa na dawa walizopewa. "Mfumo unatuwezesha kufahamu muda wa dawa kuisha matumizi yake, na unatuwezesha pia kufahamu mahitaji ya dawa kwa nyakati tofauti. Tunaweza kufahamu pia kipindi gani kunakuwa na mahitaji zaidi na ni dawa zipi, kulingana na hali magonjwa yanavyoibuka kwa kipindi fulani, mfano nyakati za mvua ambapo huwa na magonjwa ya mlipuko.

Anaongeza kwamba kwa upande wa mapato, mfumo umesaidia sana kuongeza udhibiti. Kwa kutumia mfumo unaweza kujua misamaha kwa watoto na wazee, na vilevile umeweza kuongeza makusanyo kutoka shilingi milioni 7 kwa mwezi hadi kufikia shilingi milioni 11 kwa mwezi.

Naye Afisa Muuguzi wa Kituo cha Afya cha Ngamiani, Bi Mariam Mmbaga, anasema matumizi ya mfumo wa GoT-HOMIS yamewapunguzia sana kazi kwenye eneo la kuandika kwenye makaratasi, kwa maana kila taarifa inawekwa kwenye mfumo hivyo kuwa rahisi hata kuandaa ripoti mbalimbali tofauti na hapo awali ambapo iliwalazimu kuandika kwenye makaratasi. "Hii ya kuandika kwenye makaratasi ilikuwa inatumia nija ndefu katika kukamilisha kazi, mfano ilibidi kutoa taarifa kutoka kwenye vitabu na kuandika tena kwenye makaratasi mengine," anakumbuka.

Kutoka Kituo cha Afya cha Makorora, Dkt. Masoud Adam Ntiga, Mganga Mfawidhi wa Kituo anasema kwamba mfumo wa GoT-HOMIS unasaidia sana kupunguza mianya ya upotevu wa mapato kwenye kituo chao. Kabla ya mfumo kuanza, makusanyo kwa mwezi yalikuwa shilingi milioni 5, lakini kwa sasa baada ya kuanza kutumia mfumo wa GoT-HOMISwamefanikiwa kudhibiti makusanyo hadi kufikia shilingi milioni 8 kwa mwezi.

**"**Mfumo wa GoT-HOMIS ni mzuri, ni rafiki, ni rahisi, yaani unaeleweka," anaeleza Michael Mrosso, Mfamasia wa Kituo cha Afya cha Makorora.

Mroso anaongeza kwamba kwa kupitia mfumo huu, unaweza kufahamu dawa gani ni '*fast moving*' yaani zinazotoka na kutumika mara kwa mara na wagonjwa.

"Mfumo wa GoT-HOMIS unasaidia sana kwenye udhibiti wa dawa, kwa maana huwezi kutoa dawa bila ya mgonjwa kusajiliwa na kupita kwa daktari. Na kwakuwa dawa unapokea kwa idadi tena kwa kutumia mfumo, kutoa dawa nje ya mfumo inakuwa ngumu sana kwasababu kutokuwa na taarifa sahihi ya kutoka kwenye mfumo inaleta shida kwenye ukaguzi," anaeleza.

***Inaendelea uk. 15***



***Michael Mrosso , Mfamasia wa Kituo cha Afya Makorola akiingiza taarifa kwa kutumia Mfumo wa GoT-HoMIS (Picha: Geofrey Mwaka, Tanga)***

# LAN Kuwezesha Utendaji Kazi

***Inatoka uk. 8***

"Kutokuwepo kwa mfumo madhubuti kulisababisha pia kushusha moyo watumishi wenye uzalendo, kwani hata mtu afanye kazi kiasi gani, anapokuwa haoni matokeo chanya lazima ajisikie vibaya. Kuwepo kwa mtandao kiambo utawapa ari wafanyakazi, kwakuwa sasa utendaji wao utakuwa umerahisishwa zaidi na ni rahisi kupata taarifa kwa wakati na kufanyia kazi," anaongeza Dkt. Tinuga.

Dkt. Tinuga anasema kwamba utoaji wa huduma hauwezi kuboreshwa bila ya kuwa na ongezeka la mapato na taarifa sahihi, na mfumo pekee unaoweza kuboresha taarifa ni mfumo wa GoT-HOMIS hivyo imewabidi kuthubutu kwa kuhakikisha kwamba wanafunga mfumo katika vituo vyote vya kutolea huduma. "Tunaamini huu ni mkakati ambao utatupeleka kwenye kiwango kingine, na naamini kwamba watu wanaochukua uthubutu ndio wanaofanikiwa, anasisitiza."

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ina jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 16 vya Serikali, Kati ya hivyo, vitatu ni Vituo vya Afya na 13 ni Zahanati. Mpaka kufika mwezi Septemba 2018, kila kituo cha kutolea huduma za afya cha Serikali kimefungiwa mtandao kiambo na kompyuta zaidi ya mbili kulingana na uhitaji wa kituo.

***Jacqueline Sombe, PS3***

# Matumizi ya Teknolojia Yaleta Mabadiliko

***Inatoka uk. 14***

"Kwa upande wa kitaalam mfumo umekuwa ukiboreshwa kuweza kukidhi mahitaji, kwa mfano ripoti za MTUHA ambazo mwanzoni hazikuwa zinatoka kwenye mfumo moja kwa moja kwa sasa zinatoka kwenye mfumo. Mfumo pia una uwezo wa kuhudumia wagonjwa wote walio kwenye bima na wasio kwenye bima," anasema Farida Bakari , Afisa TEHAMA wa Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Mfumo wa GoT-HOMIS unamwezesha mgonjwa kulipia gharama halisi iliyopangwa, kwa maana gharama ya kila huduma inatoka kwenye mfumo moja kwa moja na si suala la mtoa huduma kuamua bei.

Geofrey Abraham, mkazi wa Majani Mapana Jiji la Tanga anasema **"**Ingawa mimi siujui huo mfumo, lakini naona kwa sasa mambo yanaenda vizuri tofauti na hapo awali kabla ya kuwekwa hizo kompyuta maofisini. Mwanzoni tulikuwa tunaona kero kwasababu ilikuwa inachukua muda mrefu kuandikishwa, lakini madaktari wa hapa Ngamiani walikuwa wanatuelimisha kwa kutuambia mfumo ni mpya hivyo watumiaji bado hawapo vizuri sana, na tuliwaelewa. Kwa sasa naona kasi imeongezeka, bila shaka watakuwa wamekuwa wazoefu."

Geofrey anaongeza: "Tumekuwa tukisikia Rais Magufuli akitoa rai kwa wananchi pale unapolipia huduma uchukue risiti, na hapa huwa tunadai risiti na kupewa risiti zile za mashine. Binafsi nakuwa na imani kwamba hela yangu kama mlipa kodi inafanya kazi iliyokusudiwa."

Anazidi kueleza kwamba wananchi wanapolipia huduma wanataka waone kweli huduma inakuwa nzuri, na inawezekana kuwepo kwa mfumo huu ni moja ya njia ya kuboresha mapato. "*Alhamdulillah* tunaona dawa zipo, majengo yanafanyiwa ukarabati na mengine yanajengwa, tunashukuru na inatia moyo," anasema.

Matumizi ya mfumo wa GoT-HOMIS kwenye vituo vya afya na zahanati ndani ya jiji la Tanga yamekuwa na tija sana, kwani watoa huduma wa vituo vyote vinavyotumia mfumo huu wameonesha kufurahishwa na mfumo, ikizingatiwa udhibiti wa mapato na dawa, upatikanaji wa taarifa na kuwapunguzia kazi, hasa ifikapo wakati wa kuandaa taarifa mbalimbali.

***Athuman Pemba, Tanga Jiji***

# PS3, TAMISEMI Wakili wa Mfumo wa Usimamizi



***Meneja wa mifumo ya TEHAMA katika mradi wa PS3, Revocatus Mtesigwa, akikagua baadhi ya vifaa vilivyotumika katika ufungaji wa mtandao kiambo.***

*Inatoka uk. 10*

Mtesigwa anaendelea kusema kwamba mfumo unasaidia kurahisisha upatikanaji wa taarifa za Mfumo wa Takwimu wa Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA). Kutokana na hilo, kila GoT-HOMIS inavyoendelea kumuhudumia mgonjwa, taarifa za mgonjwa zinaendelea kuchakatwa moja kwa moja mpaka Wizara ya Afya kuweza kupata taarifa zote. Zamani hilo halikuwepo, lakini sasa imewezekana kwasababu GoTHOMIS "inazungumza" na mifumo mingine.

OR-TAMISEMI na PS3 imehakikisha kwamba GoT-HoMIS "inazungumza" na mifumo mingine inayohusu sekta ya afya kama vile MTUHA, Mfumo wa Uendeshaji wa Huduma za Afya (DHIS2), Mfumo wa Usambazaji Dawa (eLMIS), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), na Mfumo wa Malipo wa Kielektroniki Serikalini.

Mtesigwa anaendelea kusema kuwa kupitia mfumo "kuzungumza" na mifumo mingine, GoT-HOMIS imerahisisha kufanya usimamizi wa dawa kuanzia kujua Bohari ya Madawa inapoleta dawa, dawa gani zimetumika, na kuweza kujua dawa gani zinahitajika na zipi zimeisha muda wake wa matumizi. Hii imesaidia kuziba mianya ya upotevu wa dawa kama ilivyokuwa awali ambapo haikuwa rahisi kujua dawa kiasi gani zimepokelewa na zipi zimetumika kulingana na idadi ya watu waliohudumiwa. Upotevu wa dawa umepungua sana.

Mfumo pia umesaidia kuongeza mapato katika vituo kwakuwa sasa unaweza kujua kiasi gani kimeingizwa kutokana na malipo ya papo kwa papo, kwani hatimaye mfumo unahesabu kiasi gani kimeingia.

"Sasa hivi tuko kwenye hatua ya majaribio ya kuhuisha mfumo wa GoT-HOMIS na NHIF. Hii itawezesha kutuma taarifa moja kwa moja kupitia wagonjwa wanaotumia bima ya afya na kuweza kujua ni kiasi gani NHIF inadaiwa na kituo. Itapunguza pia mchakato mrefu ambao ulikuwa ukifanyika mwisho wa mwezi kwa kuandaa ankara nyingi kwa wakati mmoja," anaeleza Mtesigwa.

Mfumo kwa maana hiyo unawezesha ufanisi wa vituo kufanya kazi kwa kuweza kutambua historia ya mgonjwa, na unarahisisha sana kufanya utabibu kwa wagonjwa na hivyo kuchangia kuboresha huduma za afya.

Mtesigwa anamaliza kwa kusema kwamba OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na PS3 imeandaa timu ya taifa ya kiufundi ambayo itakuwa inawezesha urahisi wa utendaji kazi wa mfumo huu. Timu hii itatoa msaada pale ambapo changamoto zinatokea katika matumizi ya mfumo wa GoT-HOMIS.

***Gladys Mkuchu, PS3***